

Jina _____ Nambari _____

Sahihi ya Mtahiniwa _____

Tarehe _____

102/3
KISWAHILI
KARATASI YA 3
FASIHI
JULAI / AGOSTI 2013
MUDA: 2 ½

MTIHANI WA PAMOJA WILAYANI MAKUENI
Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari
KISWAHILI
KARATASI YA 3
INSHA
SAA : 2 ½

MAAGIZO

1. Jibu maswali manne pekee.
2. Swali la kwanza ni la lazima.
3. Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki; yaani Tamthilia, hadithi fupi, Riwaya na Fasihi Simulizi.
4. Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.
5. Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa na kuwa maswali yote yamo.

Kijitabu hiki kina kurasa 3 zilizopigwa chapa

Geuza ukurasa

SEHEMU A : USHAIRI

SWALI LA LAZIMA

1. Hisia

Ewe hisia!
Umeniamshia ndoto niloisahau zamani
Umelimsha mwangu moyoni.
Nyimbo ya kale
Na mdundo usomvutia
Ila hayawani wa mwangu rohoni.

Tulia sasa tulia
Hebu tulia ewe hisia ulo mtimani.
Nataka katu kusiona
Kwa sauti yako laini
Kwani njia zetu ni panda
Daima nazioani.

Umesubutu vipi kuniita
Kutoka mwako ngomeni
Ulimosahauliwa tangu zamani
Basi yawache maombolezi yako yaso maoni,
Yawateke hao mashujaa wa kale
Watu walo kaburini.

Hebu tulia, usiniingilie
Usinihangaishe!
Kukuandama katu haimkini
Kwani hata sasa kwa kukuwaza tu dakike hini
Naona majuto ya mbali moyoni
Kama kwamba nimegawa wangu wakati
Na wazimu, majinuni.
Basi nenda zako hisia ... shuu --- hebu tokomea.

Maswali

- (a) Huu ni utungo wa aina gani? (alama 2)
(b) Kwa kutoa mifano fafaua sifa zinaufanya utungo huu kuwa shairi. (alama 3)
(c) Eleza mawazo ya mshairi katika shairi hili. (alama 4)
(d) Dodoa mbinu nne za mtindo katika shairi hili. (alama 4)
(e) Andika ubeti wa tatu katika lugha ya nathari. (alama 4)
(f) Toa maana ya maneno haya kama yalivyotumika. (alama 3)
(i) Umesubutu
(ii) Mtimani
(iii) Moani

SEHEMU B: TAMTHILIA
TIMOTHY M. AREGE : MSTAHIKI MEYA

Jibu swali la 2 au la 3.

2. Njaa ina nguvu
Imeangusha miamba
Wenye mengi maguvu
Matata yakawakumba
Mwenye tumbo tupu
Hataki ya kuamba
Wala vitendo

- (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
(b) Hali inayolalamikiwa na msemaji imewasakama wananchi wa Cheneo vibaya. Thibitisha. (alama 10)
(c) Eleza wasifu wa msemaji na ueleze uhusika wake. (alama 6)
3. Uongozi wa Meya wa Cheneo una dosari. Thibitisha. (alama 20)

SEHEMU C : RIWAYA

Jibu swali la 4 au la 5.

4. 'Pokacha', alifanya kama anathema mate, "Juu ya ugaga wangu sijafika vile. Au unasemaje?"
- (a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)
(b) Mapenzi bandia ni jambo linalojadiliwa katika riwaya ya utengano. Fafanua dhana hii kwa kutoa hoja sita. (alama 6)
(c) Majazi ni mbinu ambayo imetumika katika riwaya ya utengano. Eleza maana ya majazi na utolee mifano mine kutoka riwayani. (alama 10)
5. "Dunia ni sumu, yafaa utahadhari." Thibitisha kauli hii ukirejelea visa mbalimbali katika riwayay ya Utengano. (alama 20)

SEHEMU D: HADITHI FUPI
DAMU NYEUSI NA HADITHI NYINGINE

Jibu swali la 6 au la 7

6. Ubaguzi na unyanyasaji ni maudhui yanayosheheni hadithi ya Damu Nyeusi. Jadili. (alama 20)
7. Hadithi ya Mke Wangu imetawaliwa na migogoro. Thibitisha. (alama 20)

SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

- (A) Taja na ueleze kwa ufupi vipera vyovyote vitatu vya maghani ya kawaida. (alama 6)
(b) Eleza sifa zozote nne za maghani. (alama 4)
(c) Fafanua mbinu tano zinazotumiwa na watafiti nyanjani. (alama 5)
(d) Kipera cha ngomezi kina sifa gani? (alama 5)

ANSWERS:

Order a copy of answers from www.schoolsnetkenya.com/order-e-copy

NB> We charge Kshs. 100 ONLY to meet website, e-resource compilation and provision costs